

KOSA LA JINAI; MAELEZO NA UFAFANUZI

Na Wakili Manace Ndoroma

Kosa la jinai ni tendo lolote ambalo limekatazwa kwa sheria, ambapo mtu yeyote akilitenda anakuwa ameikosea Jamhuri. Katika makosa ya jinai, mlalamikaji anakuwa ni Jamhuri, ikiwakilishwa na mwendesha mashitaka wa Serikali. Mtu binafisi aliyedhurika kwa tendo la kijinai siye anayeshitaki mahakamani. Yeye anabakia kuwa ni shahidi tu, na ni mara chache kwamba Mahakama inaweza kuagiza kulipwa fdia kwa mtu aliyedhuriwa na tendo la kijinai.

Katika Makosa ya Jinai, mtu anayepatikana na hatia huadhibiwa, na anayeonekana hana hatia huachiwa huru. Adhabu za makosa ya Jinai ni pamoja na: kuachiwa kwa masharti, kifungo cha nje, faini, kifungo gerezani kwa muda maalum, kifungo cha maisha na kunyongwa hadi kufa.

Makosa ya aina hii ni pamoja na wizi, mauaji, kumiliki silaha kinyume cha sheria, ubakaji, kutozingatia sheria za barabarani, nk. Makosa yote ya Jinai sharti yawe yameandikwa katika sheria mbalimbali. Hata hivyo, kwa nchi ya Tanzania, makosa mengi ya Jinai yametajwa katika Kanuni ya Adhabu (Sura ya 16 ya Sheria za Tanzania).

Mtu anayefikishwa mahakamani kwa kosa la jinai huitwa **mtuhumiwa** kwa muda wote baada ya kukamatwa, kupelekwa kituo cha polisi na hata wakati wa kujitetea mahakamani. Akishapatikana na hatia huitwa **mhalifu**, na akiadhibiwa kwa kifungo gerezani huitwa **mfungwa**.

Kimsingi, kosa lolote la jinai linakamilishwa na vitu viwili; **tendo** lenyewe lililokatazwa, na **nia ovu** ya kutekeleza tendo hilo. Mahakama inaposikiliza shauri lolote la jinai hutafuta kujiridhisha iwapo mambo yote hayo mawili yamethibitika kutokea. Katika mchakato wa kuthibitisha mambo hayo upande wa mashitaka na ule wa utetezi husikilizwa kwa makini, mashahidi huitwa mahakamani na wakati mwingine, ikibidi, vidhibiti mbalimbali huwasilishwa mbele ya mahakama ili kuthibitisha kwamba kweli tendo lililoharamishwa lilitokea, na aliyelitenda alifanya hivyo kwa makusudi

Ili Mahakama iweze kumtia hatiani mtuhumiwa sharti upande wa mashitaka uthibitishwe, bila kuacha shaka yoyote yenye mashiko, kwamba mtuhumiwa ametenda kosa ambalo ametuhumiwa nalo. Ikishindikana kuthibitisha hivyo, mtuhumiwa huachwa huru. Katika Jinai, hakuna vuguvugu wala baridi. Ni ama una hatia, au huna hatia.

Kama kosa fulani la jinai linakamilishwa na mambo matatu, ni sharti mambo yote matatu yathibitike, Upande wa mashitaka ukifanikwa kuthibitisha mambo mawili tu, basi mtuhumiwa ataachiwa huru.

Kwa mfano, kosa la mauaji linafafanuliwa kuwa ni tendo la mtu mmoja kuondoa uhai wa mtu mwingine, kwa makusudi. Maana yake ni kwamba ili mtuhumiwa athibitke kwamba aliua ni sharti kwanza mwili wa mtu aliyeuawa upatikane, ufanyiwe uchunguzi na madaktari wenye taaluma hiyo kuthibitisha kilichosababisha kifo chake, na kisha wataalamu wa masuala ya kijinai wathibitisha kwamba kilichosabaisha kifo hicho kilitendwa na mtuhumiwa, akiwa na akili timamu, na akifahamu vema matokeo ya matendo yake.

Kwa hiyo, inawezakana kwamba mtu amekufa kwa kunywa sumu iliyowekwa kwenye tunda ambalo limepakwa sumu hiyo na jirani yake, na kwamba tunda hilo baada ya kupakwa sumu liliwekwa mahali pa wazi; halikufichwa.

Iwapo mtuhumiwa atajitetea kwamba alikuwa ametega wadudu waharibifu, kama panya, na ikathibitika kwamba kweli nyumba hiyo ina panya waharibifu, mahakama inaweza kumwona hana hatia ya mauaji kwa sababu anakuwa hajakusudia kumwua mwenzake

Mambo muhimu ya kuzingatia katika somo hili ni haya:

- (a) Kila kosa la jinai limeandikwa katika kitabu cha Sheria
- (b) Mtu yeyote hataitwa mhalifu mpaka pale atakapothibitika kuwa ametenda kosa la jinai
- (c) Kosa la jinai lazima lithibitike bila kuacha shaka yoyote yenye mashiko
- (d) Kosa la jinai lina pande mbili; kutenda jambo lililokatazwa na nia ya kutenda jambo lililokatazwa
- (e) Mwathiriwa wa kosa la jinai ni shahidi wa upande wa mashitaka, si mshitaki

Tukutane katika somo lijalo!